



# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-28 FEBRUARI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 MACHI, 2025**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-28 FEBRUARI, 2025**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la kaskazini magharibi mwa bahari ya Hindi (Pwani ya Somalia) lilikuwa la chini ya wastani. Hali hii ilipelekea upepo mkavu kutoka kaskazini mashariki kuelekea maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-28 FEBRUARI, 2025**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa Hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki na maeneo ya ukanda wa pwani; ngurumo za radi katika maeneo machache ya kusini mwa nchi; na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 MACHI, 2025**

### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 MACHI, 2025**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kutokuwa na mabadiliko wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kudhoofika kidogo. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo na kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu hasa yale yaliyopo nyanda za juu kusini-magharibi, kanda ya magharibi, kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la kaskazini magharibi mwa bahari ya Hindi (Pwani ya Somalia) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo mkavu kutoka kaskazini mashariki kuelekea maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, nyanda za juu

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

kaskazini mashariki na maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo hususani katika nusu ya kwanza ya dekad.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 MACHI, 2025**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):**

Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika katika maeneo machache ya mkoa wa Kigoma na hali ya ukavu kiujumla inatarajiwa katika maeneo ya mikoa Katavi na Tabora.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

### **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

---

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)